2022
2023



# HAKI ZA MWANAFUNZI

# & MAJUKUMU YAKE

LEARNING FOR A LIFETIME
SALEM•KEIZER PUBLIC SCHOOLS

Christy Perry, Superintendent

Salem-Keizer Public Schools 24J does not discriminate on the basis of race, color, national origin, sex, disability or age in its programs and activities.
This policy implements state and federal laws (including Title IX); inquiries about the non-discrimination policies should be directed to the Compliance Officer, Executive Director in the Human Resources Office, 2450 Lancaster Dr. NE, Salem, OR 97305. Phone: 503-399-3061

Rev. 9/2022 INS-M001

[redacted]

Kwa zaidi ya miaka miwili, Salem-Keizer imejidhatiti kutengeneza mazingira salama na ya ukaribisho shuleni. Kama sehemu ya huu mchakato, tumebadilisha mfumo wa tabia na kuwa wa ujumuisho pamoja na usawa, kuweka mkazo kwenye kusoma na kukuwa. Shukruani kwa Wataalamu wa Tabia na Uongozi kwa kazi yao ya kiundani ya mwaka jana, tumetengeneza Falsafa ya Tabia Inayofanyakazi hapo chini. Kipindi chote cha Fall ya mwaka 2021, tutakusanya taarifa kutoka kwa wanafunzi, familia na wadau wa jamii na kuwaataarifu mwisho wa toleo ambalo litachapishwa Januari ya mwaka 2022. Wakati tunarejesha mfumo wa tabia, wanafunzi wanaweza kushuhudia majibu kutoka kwa wafanyakazi yanayoendana na msaada wakinidhamu uliopo. Tutaendelea kufanyakazi ya kutekeleza mazoea na adhabu ambayo yanalenga kurudisha mahusiano yalioathiriwa, kupunguza tabia ambazo zinaweza kujirudia na kuimirisha ujuzi muhimu kustawi.

<u>Kauli ya Falsafa ya Tabia Inayofanya Kazi Shule za Umma za Salem Keizer (SKPS)</u>

Tunaamini wanafunzi wetu na kuwahamasisha kuwa salama na kufanya maamuzi salama kulingana na tabia. Wakati tukio likitokea, wanafunzi, wazazi/mlezi na wafanyakazi wa shule wanakaribishwa kwa ushirikiano kutafuta uelewa wa tukio, na kufanya kazi pamoja kwa kujifunza na kutengeneza mahusiano na madhara yote ya tukio

SKPS watatumia kwa ufanisi uzoefu wa shule kuhakikisha mazingira ya shule ni muafaka kwa kusoma, na kuwakikisha usalama na ustawi wa wanafunzi na wafanyakzi. Kwa kuongezea, wilaya imejidhatiti kuondoa tofauti na zisizo za uwiano kwa kutengeneza utamaduni wa shule ambapo matarajio ya kuwa ya uwazi yanafundishwa kuendana na kuimarishwa kwa kutoa mazingira ambayo wanafunzi wote wanajisikia kuungana, salama, kusaidiwa, kuthaminiwa na kusikikia.

Mazoea ya tabia zenye mafanikio yana sifa zifuatazo:

1. Vinatazamwa kama fursa ya kusoma, kubuni kufundisha, kutambua, na kuhamasisha tabia nzuri.
2. Zinahakikisha fursa kwa wanafunzi katika kupata elimu, kuweza mkazo wa kushiriki wanafunzi darasani.
3. Wanaitikia kiutamaduni kwa kutafuta kuelewa kiundani na kuheshimu kila mali na maadaili ya kitamaduni ya mwanafunzi.
4. Ziko wazi na zinafaa kwa wakati.
5. Zinajumuisha aina mbalimbali za kuzuia na vipimo vya uingiliaji.
6. Zinatoa fursa kwa wafanyakazi, wazazi/familia na wanafunzi kushiriki.
7. Wana mantiki, usawa, thabiti, inayofaa kimaendeleo, na zinazojali hali.
8. Wana tambua na kuzingatia tofauti ya mtu binafsi kati ya wanafunzi wenye ufahamu na fikra.
9. Wanaongeza ufahamu wa wanafunzi na athari za tabia zao kwa kutoa fursa ya kutafakari na kurekebisha uhusiano unaofaa.
10. Kujenga hali ya jamii kwa kungeza uwezo wa jamii kwenye kutatua migogoro, wakati wanalinda tamaduni za mazingira mazuri ya shule.

***(Maelezo ya Wilaya kwenye Sera na Utaratibu wa Nidhamu unapatikana katika kila ofisi ya wilaya au kwenye tuvuti ya wilaya)***

Hizi ni sera na utaratibu uliowekwa kulinda usalama, haki na majukumu ya wanafunzi, wazazi na wanafanyakazi. Hizi zinahusu mwenendo wa mwanafunzi ambao hutokea wakati mwanafunzi yuko:

1. Kwenye maeneo ya shule kabla, wakati au baada ya muda wa shule.
2. Kwenye matukio yanayodhaminiwa na shule kabla, wakati au baada ya kumaliza muda wa shule kujumuisha safari na shughuli zinazodhaminiwa na shule kwenye mji mwingine, jimbo au nchi.
3. Kusafiri Kwenda na kurudi kwenye shughuli zinazodhaminiwa na shule.
4. Kwenye maeneo ya shule wakati wowote shule inatumiwa na wanadhamini wa matukio.
5. Kujiunga na shule za summer na /mwingiliano.
6. Kwenye maeneo nje ya shule wakati vitendo vinahusishwa kutishia au kuumiza wanafunzi, wafanyakazi na/au mali za wilaya.

Kwa kuongezea mwanafunzi anaweza kupewa rufaa kwa mshauri wa shule, timu ya CARE, Timu ya huduma kwa vijana au Timu inayotathimini. Ifuatayo ni orodha pana ya tabia zote ambazo zinaweza kuhitaji nidhamu lakini inaeleleza uangalifu kwa baadhi ya mifano ya madhumuni ya vielezo.

| KOSA | **MLOLONGO UNAOENDELEA WA MATOKEO**<br>*Kiwango chochote cha matokeo kinaweza kusimamiwa kwa kosa lolote na kwa kuzingatia umri na tabia ya awali ya mwanafunzi.* |
|---|---|
| **Kuumizwa Kimwili** – Kwa kukusudia, kujua au bila kujali na/au kusababisha maumivu kwa mtu mwingine.<br><br>**Tabia ya Fujo** – Kupigana kuliko elekezea mtu mwingine, kujumuisha na siyo tu, kupiga teke, kupiga, kung'ata, kusukuma, kuangusha, kupiga kofi au kujaribu kumuumiza. | • Mwanafunzi ambaye amemuumiza mwenzake hatarudi darasani mpaka adhabu aliyopangiwa kukamilika na anaweza kupangiwa darasa lingine, darasa au shule.<br>• Wasiliana na mzazi au mlezi<br>• Kusimamishwa mpaka siku 10. Kwa wanafunzi wa darasa la 5 au chini, pitia sehemu ya kipengele 3.3.3 ya Nidhamu: Wanafunzi INS-P028.<br>• Urejeshaji.<br>• Rufaa kwa vyombo vya sheria.<br>• Kuendelea kusimamishwa na mapendekezo ya kufukuzwa.<br>• Uchunguzi wa (afya ya akili, ushauri) kwa gharama za wazazi. |
| **Tishio** – Kumweka mtu mwingine kwenye hofu ya madhara ya kimwili kwa maneno (kuandikia au kuongea) au mwenendo.<br><br>**Uonevu, Bullying, Unyanyasaji Harassment & Vitisho** –Kitendo chochote kinachoingiliana na fursa ya elimu kwa mtu au utendaji; unaotokea maeneo ya shule, katika shughuli zinazodhaminiwa na shule, kwenye usafiri unaotolewa na shule au kwenye kituo rasmi cha basi la shule; na hiyo inamadhara kujua kumuweka mtu kwenye wasiwasi wa kuumizwa au hofu ya kurudhishwa kwamba uharibifu unaweza kutokea kwa mali ya mtu au kuunda mazingira ya kielimu yenye uadui ambayo yataleta huzuni, vitisho, kudhalilisha, kuudhi au kutesa mtu mwingine.<br><br>**Unywanywasi wa Kijinsia** – Ombi la ngono lisilokubalika la upendeleo wa ngono na mwenendo mwingine wa kimaandishi au wa kimwili na asili ya ngono ambao unaingiliana bila sababu ya elimu ya mtu na/juu ya ushiriki wa mtu katika shughuli za shule au unaozua uhasama wa kutisha au wa kukera shuleni.<br><br>**Unyanyasaji wa Ubaguaji** – Imani ya kwamba wanachama wa rangi moja ni bora zaidi kuliko wanachama wa rangi nyingine au kundi la asili na kutumia maneno, na/au hatua za kutekeleza hizo imani. | • Wasiliana na mzazi au mlezi.<br>• Mkutano wa usimamizi wa mgogoro.<br>• Usimamishwaji ukiwa shuleni na mradi maalumu.<br>• Kusimamishwa mpaka siku 10. Kwa wanafunzi wa darasa la 5 au chini, pitia sehemu ya kipengele 3.3.3 ya Nidhamu: Wanafunzi INS-P028.<br>• Rufaa kwa vyombo vya sheria.<br>• Mkutano pamoja na mzazi kabla ya mwanafunzi kurudi shuleni.<br>• Kuendelea kusimamishwa na mapendekezo ya kufukuzwa.<br>• Uchunguzi kwa gharama za wazazi. |
| **Tabia ya Kutokutii** – Tabia ya kutokutii imefafanuliwa na inaweza kujumuisha, lakini siyo tu: kutotii au kukaidi watumishi wa wilaya na mamlaka; kwa maneno, kimwili, na/au lugha chafu au tabia mbaya, kusumbua darasa lolote, shule au shughuli zinazodhaminiwa na wilaya; tabia inayoelekezea hatari kwa mwanafunzi au wengine; Kwa makusudi na/au kujua kusambaza video au picha za mwanafunzi ambaye tabia haiendani na sheria na miongozo ya shule na/au marejeleo mengi kwa mwenendo kwa kutotii. Tabia zisizo salama wakati wa usafiri wa basi la shule kutoka shule na kurudi au kwenye matukio yanayodhaminiwa na shule. | • Kuondolewa darasani au kwenye shughuli zote zote za wilaya<br>• Wasiliana kwa ajili ya mkutano wa wazazi au mlezi<br>• Kizuizini, kwa kusimamishwa shule<br>• Kusimamishwa shule hadi siku 10 za shule, kuwa na mradi maalumu au kusimamishwa shule na kuruhusiwa kuwa shule kwa mradi maalumu. Kwa wanafunzi wa darasa la 5 au chini, pitia sehemu ya kipengele 3.3.3 ya Nidhamu: Wanafunzi INS-P028.<br>• Kuendelea kusimamishwa na mapendekezo ya kufukuzwa. |
| **Silaha** – Umiliki, kusambaza, kuuza au kwa njia yoyote kuonyesha silaha, vifaa, chombo, nyenzo au dutu, bunduki, vilipuzi haramu, au chombo kingine ambacho kinaweza kutumika kama silaha, au kujaribu kutumika kama silaha au kutishia kunaweza kutumika kama silaha au ana uwezo wa kusababisha kifo au majeraha makubwa ya kimwili na au ambayo hayana matumizi yeyote ya kuridhisha au ya kielimu kwa mwanafunzi. | • Kunyang'anywa kwa kitu kinachohusiana na kosa.<br>• . Mkutano pamoja na mzazi au mlezi.<br>• Rufaa kwa mamlaka ya vyombo vya sheria.<br>• Kuendelea kusimamishwa na mapendekezo ya kufukuzwa. |

| | |
|---|---|
| **Inayofanana kama Silaha** – Umiliki, kusambaza, kuuza, au kuonyesha kifaa chochote, nyenzo au zana nyingine ambayo inaweza kuzingatiwa kuwa silaha kama inavyofafanuliwa katika sera na/au ambayo haina matumizi ya kuridhisha au ya kielimu kwa mwanafunzi. | • Kunyang’anywa kwa kitu kinachohusiana na kosa.<br>• Wasiliana kwa ajili ya mkutano wa wazazi au mlezi.<br>• Kusimamishwa shule lakini bado uko shuleni.<br>• Kusimamishwa shule hadi siku 10 za shule. Kwa wanafunzi wa darasa la 5 au chini, pitia sehemu ya kipengele 3.3.3 ya Nidhamu: Wanafunzi INS-P028.<br>• Rufaa kwa vyombo vya sheria.<br>• Kuendelea kusimamishwa na mapendekezo ya kufukuzwa. |
| **Pombe na Madawa Mengine** – Umiliki, kununua, kutumia, au kuwa chini ya ushawishi wa pombe; kuvuta kujumisha na vimumunyisho na madawa mengine; au dawa nyingine zinazotambuliwa na siyo tu kwenye Uniform Controlled Substance Act, ORS 475.005; umiliki wa paraphernalia, umiliki unaofanana kama dawa zinazozibitiwa na/au matumizi mabaya ya dawa au dawa zisizohitaji kuandikiwa na daktari. | • Kunyang’anywa kwa kitu kinachohusiana na kosa.<br>• Wasiliana kwa ajili ya mkutano wa wazazi au mlezi<br>• Rufaa kwa mamlaka ya vyombo vya sheria.<br>  • Kusimamishwa shule nje au ndani mpaka siku 10 za shule. Kwa wanafunzi wa darasa la 5 au chini, pitia sehemu ya kipengele 3.3.3 ya Nidhamu: Wanafunzi INS-P028.<br>  • Rufaa kwa mamlaka ya vyombo vya sheria.<br>• Kuendelea kusimamishwa na mapendekezo ya kufukuzwa. Kwa wanafunzi wa darasa la 5 au chini, pitia sehemu ya kipengele 3.3.3 ya Nidhamu: Wanafunzi INS-P028. Pendekezo linawezekana la kugeuza. |
| **Pombe na Madawa Mengine** – Kuuza, kusambaza au umiliki kwa nia ya kuuza pombe, kuvuta, kujumisha na vimumunyisho na madawa mengine; au dawa nyingine zinazotambuliwa na siyo tu kwenye Uniform Controlled Substance Act, ORS 475.005, kujumuisha zile zinazofanana kama dawa zinazozibitiwa na/au matumizi mabaya ya dawa au dawa zisizohitaji kuandikiwa na daktari. | |
| **Tumbaku au Bidhaa ya Tumbaku** – Kuvuta, umiliki, kuuza, kununua, kuhamisha, kusambaza, au kutumia tumbaku au bidhaa ya tumbaku. Hii inajumuisha vile vinavyofanana na tumbaku na bidhaa za tumbaku na vitu vya kuwakilishwa kama tumbaku na bidhaa za tumbaku (kama vile sigara na yaliyomo). | • Kunyang’anywa vitu vyovyote vinavyohusiana na kosa.<br>• Wasiliana kwa ajili ya mkutano wa wazazi au mlezi.<br>• Mradi maalumu kama ilivyoagizwa na msimamizi.<br>• Kusimamishwa, nje au ndani ya shule mpaka siku (3Kwa wanafunzi wa darasa la 5 au chini, pitia sehemu ya kipengele 3.3.3 ya Nidhamu: Wanafunzi INS-P028.<br>• Rufaa kwa mamlaka ya vyombo vya sheria. |
| **Mahudhurio – Kutokuhudhuria bila ruhusa**–Kutokuhudhuria darasani bila ruhusa kutoka kwa mzazi na mlezi. | • Wasiliana na mzazi au mlezi.<br>• Uundaji wa mkataba wa mahudhurio utakaoamuliwa na msimamizi wa shule.<br>• Kuzuiliwa au kusimamishwa shule.<br>• Rufaa kwa mamlaka ya vyombo vya sheria.<br>• Kubakizwa/Kushindwa kupokea alama kwa kazi ya shule. |
| **Mahudhurio – Kuchelewa** – Kutokuhudhuria darasani bila ruhusa kutoka kwa mzazi na mlezi . | • Wasiliana na mzazi au mlezi.<br>• Uundaji wa mkataba wa mahudhurio utakaoamuliwa na msimamizi wa shule.<br>• Kuzuiliwa au kusimamishwa shule .<br>• Retention/failure to receive credit for course work Kubakizwa/Kushindwa kupokea alama kwa kazi ya shule. |
| **Kuwasha moto** – Kitendo chochote au jaribio la kuwasha moto | • Kunyang’anywa vitu vyovyote vinavyohusiana na kosa.<br>• Wasiliana kwa ajili ya mkutano wa wazazi au mlezi.<br>• Rufaa kwa mamlaka ya vyombo vya sheria.<br>• Urejeshaji. |

| | |
|---|---|
| | • Kuondolewa kwenye ushiriki shughuli za shule mpaka urejeshwaji ufanyike<br>• Kusimamishwa shule nje au ndani mpaka siku 10 za shule. Kwa wanafunzi wa darasa la 5 au chini, pitia sehemu ya kipengele 3.3.3 ya Nidhamu: Wanafunzi INS-P028.<br>• Kuendelea kusimamishwa na kushauri kufukuzwa. |
| **Mtandao wa Kompyuta na Mtandao** –Matumizi mabaya au matumizi ya mitandao na/mfumo wa mtandao kutishia kuharibu mali za wilaya au mtu au hujuma au kurekebisha programu za wilaya, kompyuta za wilaya mitandao na/au mfumo wa mtandao kama inavyoelezea kwenye sera za Wilaya INS A004. | • Wasiliana na mzazi au mlezi.<br>• Kusimamishwa au kubatilisha haki za mfumo wa upendeleo kwa wastani wa siku 30 za kalenda.<br>• Kusimamishwa shuleni kusimamishwa shule mpaka siku 10 za shule. Kwa wanafunzi wa darasa la 5 au chini, pitia sehemu ya kipengele 3.3.3 ya Nidhamu: Wanafunzi INS-P028.<br>• Ubatilishaji wa kudumu kwa mfumo wa upendeleo.<br>• Rufaa kwa vyombo vya sheria.<br>• Kuendelea kusimamishwa na kushauri kufukuzwa. . |
| **Uharibifu wa Mali na Wizi** –Uharibifu wa makusudi na mali za wilaya na/au wizi wa mali ya wilaya au kwa mtu mwingine, kujumuisha na siyo tu lakini pia utunzaji usiofaa wa vitabu, kabati na kufuli. | • Wasiliana na mzazi au mlezi.<br>• Urejeshaji<br>• Kusimamishwa shule.<br>• Kusimamishwa shule mpaka siku 10. Kwa wanafunzi wa darasa la 5 au chini, pitia sehemu ya kipengele 3.3.3 ya Nidhamu: Wanafunzi INS-P028.<br>• Kutokushiriki shughuli za shule mpaka urejeshwaji ufanyike<br>• Kuendelea kusimamishwa na kushauri kufukuzwa.<br>• Rufaa kwa mamlaka ya vyombo vya sheria.<br>• Uchunguzi kwa gharama za wazazi. |
| **Kutokulipa ada, faini, na/au kurejeshwa kwa mali iliyoharibiwa au kupotea.** | • Wasiliana na mzazi au mlezi.<br>• Rufaa kwa wakala wa ukusanyaji na au utekelezaji wa sheria. |

## KUSIMAMISHWA

Kusimamishwa ni kuondelewa kwa mwanafunzi shuleni kutoka katika majengo/mali na ushiriki na/mahudhurio katika au kwenye shughuli za shule au kwenye matukutio yanayodhaminiwa na shule kujumuisha michezo na upatikanaji wa usafiri, na kwa siku siyo zaidi ya kumi za shule.

Kama mwanafunzi, mzazi au mtu mwingine mwenye mahusiano ya wazazi atakuwa na siku mbili za kutoka kwa uamuzi wa shule na kusimamishwa ambapo atakata rufaa kwa Mkuu wa mashule au mtu aliyeteuliwa

Mkuu wa mashule au mteuliwa atapitia rekodi ya maandishi na/au anaweza kusikiliza usikilizaji usio rasmi na kutoa maamuzi ya maandishi ndani ya siku (3) za shule kutoka kwenye notisi ya rufaa. Kama mwanafunzi, mzazi au mtu mwingine mwenye mahusiano ya wazazi anaweza kukata rufaa ya maamuzi ya Mkuu wa mashule au aliyeteuliwa kwa Bodi ya shule ndani ya siku (2) za shule kutoka walipopokea maamuzi.

## KUFUKUZWA

Mwanafunzi yeyote aliyekiuka sera na utaratibu wa wilaya anaweza kufukuzwa. Kufukuzwa ni kuondolewa kwenye Bodi ya Shule au mteule wake wa mwanafunzi kutoka katika majengo ya shule/mali, usafiri wa shule, na katika kushiriki shughuli za shule na siyo zaidi ya mwaka mmoja wa kalenda

Kama mwanafunzi anaulemavu na/au wanafunzi wako kwenye uchunguzi wa elimu maalumu na kama ametenda kosa na kufukuzwa ni mapendekezo ya hatua za kinidhamu, kabla ya mabadiliko haya ya uwekaji uamuzi utafanywa kubaini kama utovu wa nidhamu wa mwanafuzni umesababishwa na ulemavu au uwekaji usiofaa.

Mwanafunzi ambaye imependekezwa kufukuzwa shule atasikilizwa mbele ya afisa wa kusikiliza; itasikilizwa kufuatana na ORS 332.061 na kulingana kwa sera na utaratibu wa wilaya kama inavyoweza kuelekezwa na Mkuu wa mashule.

Mwanafunzi anaweza kuwakilishwa na mshauri wa sheria au mtu mwingine kwa gharama za mwanafunzi. Mwanafunzi, mzazi au mtu mwingine mwenye mahusiano ya wazazi anaruhusiwa kukagua kabla ya kusikilizwa, hati za kiapo au vielelezo ambavyo wilaya inakusudia kuwasilisha kwenye usikilizaji. Mwanafunzi ataruhusiwa kuwasilisha ushahidi kwa maandishi ya ushuhuda au maonyesho mengine. Kesi itaamuliwa tu kwa ushahidi uliotelewa kwenye usikilizwaji. Afisa anayesikiliza atatoa uamuzi kwa maandishi ndani ya masaa 24 ya kusikilizwa.

Ndani ya siku tano za shule baada ya kupokea uamuzi wa awali wa afisa kusikiliza au siku saba za kalenda na kama uamuzi wa

ya fomu ya Notisi ya Kukata rufaa iliyotengenezwa na ofisi ya Mkuu wa mashule. Rufaa itawasilishwa na ofisi ya Mkuu wa mashule.

## MUACHANO

Baada ya mapendekezo ya uongozi wa shule, mwanafunzi ambaye amekiuka sera ya silaha au madawa/pombe au sheria inaweza kumpa fursa ya kushiriki katika programu ya Diversion.

## ELIMU MBADALA

[redacted]

kufukuzwa shule baada ya shule kuisha mwishoni mwa Juni, mzazi au mtu mwingine mwenye mahusiano ya wazazi, au mwanafunzi kama ana miaka 18 au zaidi anaweza kuomba Bodi ipitie maamuzi

## MKUSANYIKO WA WANAFUNZI

Wilaya ya shule za Salem-Keizer inatambua haki ya katiba ya wanafunzi kukusanyika. Hata hivyo, ifahamike kuwa shule nyingi zimejaa wanafunzi, kutokana na ufinyu wa nafasi. Mkusanyiko wa wanafunzi unatakiwa uendane na programu za shule, na siyo kuvuruga masomo na isisababishe madhara kwa watu au mali. Mkusanyiko wa mwanafunzi maombi yapelekwe mapema kwa mkuu wa shule, na wanafunzi watapelekewa taarifa ya maamuzi ndani ya wakati unaofaa.

## BAISKELI, UBAO WA KUENDESHA & SKUTA

Mwanafunzi yeyote anaweza kuendesha baiskeli shuleni. Ingawa, mwanafunzi atakayeendesha baiskeli shuleni lazima kujua na kufuata sheria za usalama na kuonyesha tabia nzuri ya kuendesha. Ufuatao ni mwongozo wa ziada sheria za kawaida za kuendeshea baiskeli salama:

1. Sheria ya Oregon kwenye kuvaa kofia ya kuendeshea baiskeli ORS 814.485 inataka kila mtoto mpaka miaka 15 kuvaa kofia ya kuendeshea baiskeli iliyothibitishwa wakati unaendesha sehemu yoyote ya wazi ya umma – njiani, barabarani, upande wa watembea kwa miguu, na sehemu za kuchezea.
2. Baiskeli hazitakiwi kuendeshwa kwenye maeneo ya shule wakati wa muda wa shule au wakati wa shughuli za shule baada ya shule.
3. Kuendesha wawili kwenye baiskeli hairuhusiwi.
4. Adhabu kwa kuendesha bila kufuata sheria au kushindwa kunaweza kutambuliwa na mkuu wa shule, wafanyakazi wa shule, au wazazi.
5. Wanafunzi wanashauriwa kufunga baiskeli zao kwenye sehemu za kuhifadhia. Wakati jitihada zote zinatolewa kuhifadhi baiskeli wakati wa masomo, wanafunzi wanatakiwa kujua kwamba wanapoleta baiskeli wanabeba dhamana.

Kila mwanafunzi anaweza kuendeshea ubao wa kuendeshea au skuta, ingawa wanafunzi wanaoendesha ubao wa kuendeshea au skuta shuleni lazima kujua kufuata sheria za usalama na kuonyesha

Wanafunzi waliofukuzwa kutoka kwenye wilaya atataarifiwa kwa programu ya elimu mbadala iliyotengenezwa kutoa aina mbalimbali za mazingira, wakati, muundo na/au mbinu za kufundishia na ambazo anaweza kushiriki akiwa amefukuzwa.

tabia nzuri ya kuendesha. Ufuatao ni mwongozo wa ziada, sheria za kawaida za kuendesha baiskeli salama:

1. Sheria ya Oregon ya kuvaa kofia wakati wa kuendesha ubao wa kuendeshea na skuta ORS 814.600 inataka kila mtoto mpaka miaka 15 kuvaa kofia za kujikinga.
2. Ubao wa kuendeshea na skuta haviendeshwi kwenye ardhi ya shule muda wowote. Mara unapofika kwenye maeneo ya wilaya, mwendeshaji anatakiwa kubeba ubao na kutembea.
3. Ubao wa kuendeshea na skuta haviendeshwi karibu na mabasi ya shule.
4. Adhabu ya kutokuendesha salama au kushindwa kufuata sheria inaweza kutolewa na mkuu wa shule au mfanyakazi wa shule.

## KAMPASI KUFUNGWA

Shule za Wilaya ya Salem-Keizer zinazuia wanafunzi kwenye maeneo ya shule wakati wa masomo isipokuwa pale tu. Wanafunzi wote watabakia kwenye maeneo ya shule mara wanapowasili wakati wa asubuhi mpaka muda wa kuruhusiwa mwisho wa siku. Haya mahudhurio yanahitajika kujumuisha muda wa saa moja mchana isipokuwa zifuatazo: Kwenda na kurudi nyumbani kwa mapumziko ya chakula kama alivyoomba mzazi; kwenda kufuatilia kitu au kwenye miadi kama ilivyoombwa na mzazi; na kufanya programu ya shule iliyopangwa na shule kama kujisomea au kazi. Mwanafunzi anayetaka kuondoka kampasi wakati wa shule lazima kupata kibali kutoka kwa uongozi wa shule.

Kufunguliwa kwa kampasi (INS-P024) au muda wa chakula cha mchana usio na kikomo kwa wanafunzi wanahudhuria high skuli za Salem-Keizer ni wa upendeleo na kuamuliwa kila mwaka kulingana na maombi ya baraza la wanafunzi na hatua za high skuli kwenye ngazi ya ukurugenzi.

## MCHAKATO WA MALALAMIKO (ADM-A005)

Shule za Wilaya ya Salem-Keizer imejidhatiti kutatua matatizo kwa muda muafaka, moja kwa moja, kwa maongezi yasiyo rasmi, kuanzia na shule au idara husika. Mawasiliano ni muhimu wakati wa mchakato ili makundi yanayohusika waweze kuelewa sababu

nyuma ya msimamo wa kila mmoja. Pale itakapowezekana, malalamiko yanatakiwa kutumwa na kuelezewa katika shule au idara na kupitia njia inayotambulika kama inayoenyesha kwenye Mchakato wa Malalamiko ya Wilaya (ADM-P008). Mchakato wa malalamiko upo kwenye tuvuti ya wilaya. Wilaya ya Shule za Salem-Keizer, sera inakataza kulipiza kisasi au kumlipizia kisasi mtu yeyote anayetenda kwa nia njema katika mchakato wa malalamiko.

## MWENENDO KWENYE MABASI YA SHULE

Wanafunzi wanaotumia usafiri wa wilaya wanatakiwa kufanya hivyo kwa mwenendo wa Utaratibu wa Wilaya TRN-P036. Kuendelea kutumia usafiri wa wilaya ni kulingana na uzingatiaji wa wanafunzi kwa Sera na Utaratibu wa Nidhamu wa Wilaya.

## MZAZI MLEZI NA ASIYE MLEZI

Wilaya itatoa haki zote chini ya utaratibu INS-P022, Rekodi ya mwanafunzi kwa mzazi yeyote, au mtu mwenye mahusiano ya mzazi, labda tu wilaya imepokea ushahidi wa maandishi kuonyesha kuwa kuna amri ya mahakama, sheria ya serikali, au hati ya kisheria kuonyesha mambo kama kuachana, kutengana au mzazi mlezi ambayo haswa itabatilisha haki hizi. Mzazi asiye mlezi anatakiwa kuwapatia shuleni anuani ili taarifa za shule ziweze kutumwa.

ORS 107.154(1) na (4) inatamka kwamba isipokuwa kama itaamriwa vinginenyo na mahakama amri ya mlezi pekee kama mzazi mmoja haitamnyima mzazi mwingine mamlaka yafuatayo:

- Kukagua na kupokea rekodi za shule na kuwasiliana na mfanyakazi wa shule wasiwasi wa maendeleo ya elimu, kama mzazi mlezi anavyoweza kukagua na kupokea hizi rekodi na kushaurina na wafanyakazi.
- Kuruhusu matibabu ya dharura, meno, ushauri wa kisaikolojia, kiakili au mambo mengine ya afya kwa mtoto kama mzazi mlezi, na madhumuni ya vitendo, hayapo. Mwanafunzi hataruhusiwa kuchukuliwa na mtu anayesema yeye ni mzazi mlezi wa mwanafunzi labda tu huyo mtu awe ameorodheshwa na mzazi mlezi au anaweza kutoa utambulisho binafsi na amri ya ulinzi wa kisheria iliyotolewa na Jimbo la Oregon

## SERA ZA UVAAJI (INS-A025)

Shule za Umma za Salem-Keizer zinategemea wanafunzi wote watavaa nguo za heshima kwa ajili ya shule siku nzima au kwenye shughuli zinazodhaminiwa na shule. Uchaguzi wa mavazi ya wanafunzi unapaswa kuheshimu nia ya kuendeleza jumuiya inayojumuisha aina mbalimbali za utambulisho. Jukumu la kwanza kwa mavazi ya wanafunzi ni mwanafunzi na wazazi au walezi.

Wilaya ya shule inajukumu la kuona mavazi ya shule hayaingiliani na afya au usalama wa wanafunzi, ya kwamba mavazi ya mwanafunzi hayachangii hali ya uhasama au ya kutisha kwa mwanafunzi yeyote, na kwamba utekelezaji wa kanuni za mavazi hauimarishi au kuongeza kutengwa au ukandamizaji wa kikundi chochote kwa msingi wa rangi, jinsia, utambulisho, jinsia kujieleza, mwelekeo wa kijinsia, kabila dini, uzingatiaji wa kitamaduni, mapato ya familia au aina ya mwili/ukubwa.

Vizuizi vyovyote vya jinsi mwanafunzi anavaa lazima kiwe muhimu ili kusaidia malengo ya jumla ya elimu ya shule na lazima ifafanuliwe ndani ya kanuni hii ya mavazi. Kwa taarifa zaidi tafadhali pitia Sera ya Uongozi INS-A025 kwenye tuvuti ya wilaya.

## VIFAA VYA KIELEKTRONIKI

Vifaa vya kielektroniki vinaweza kuleta usumbufu na kuvuruga mazingira ya kujifunzia shuleni. Vifaa hivi ni pamoja na, na haviishii tu kwenye simu za mkononi, saa, vya kusikilizia/vya kuvaa vichwani kwa ajili sauti, kompyuta kibao, na michezo ya kielektroniki na vifaa vinavyoingilia mazingira ya kujifunzia. Matumizi na upatikanaji wa rasilimali za kielektroniki (ikiwa ni pamoja na simu za mkononi) zitatofautiana kulingana na kile kinachofaa kimaendeleo kwa kiwango cha darasa la wanafunzi, kiwango ambacho upatikanaji huu unaweza kusaidia mazingira ya elimu kwa mwanafunzi, na usumbufu unaoweza kutokea kama matokeo ya kutumia mwanafunzi. Matokeo yake, miongozo ifuatayo ya sera itatungwa kwa kila ngazi ya darasa.

High skuli: Wanafunzi wanaweza kutumia simu za mkononi katika maeneo ya kawaida (kama sehemu ya kulia chakula) na wakati wa kubadilisha madarasa. Matumizi ya simu za mkononi darasani wakati mwalimu anafundisha zitatumika kwa madhumuni ya taaluma na maamuzi yatakuwa ni ya shule.

K-8: Wanafunzi wanaweza kutumia simu za mkononi kabla na baada ya muda wa shule. Wakati wa masaa ya shule wanafunzi hawaruhusiwi kutumia simu zao madarasani, maeneo ya kawaida (chakula cha mchana) au wakati wa kubadilisha masomo. Matumizi ya simu za mkononi wakati wa ufundishaji darasani hasa kwa madhumuni ya kitaaluma utakuwa uamuzi wa shule kuruhusu tu na kwa wakati hali fulani. Kwa ujumla, wanafunzi watatakiwa kuzima simu zao za mkononi na kuziweka ndani ya mikoba yao, au na ofisi au kabati lao la kuhifadhia (likiwa inapatikana).

Wazazi wanaohitaji mawasiliano ya haraka na mwanafunzi wao wanaombwa kupiga simu ofisi ya shule hiyo. Wilaya haihusiki na usalama, msaada, tozo za matumizi, uharibifu, au wizi wa vifaa binafsi vya kielektroniki.

## RASILIMALI ZA KIELEKTONIKI NA MTANDAO (INS-A004)

Mwanafunzi chini ya umri wa miaka 18 anaweza kutumia rasilimali za kielektroniki, ikiwa ni pamoja na mtandao, katika shule za Salem-Keizer isipokuwa kama mzazi wake au mtu mwingine katika uhusiano wa wazazi anakataa mwanafunzi kupata kupitia ukukamilishaji wa fomu ya kutengwa (INS-F048). Wilaya inaweza kusimamisha au kufuta upatikanaji wa mtumiaji kwa rasilimali za kielektroniki na/au mtandao na inaweza kutoa taarifa za ukiukwaji kwa mamlaka za utekelezaji wa sheria endapo mtumiaji atakiuka Sera ya Wilaya.

## FURSA SAWA YA ELIMU KWA WANAFUNZI WOTE (ADM-A009)

Ni sera ya Wilaya ya Shule ya Salem-Keizer kwamba hakuna mwanafunzi aliyeandikishwa katika wilaya hiyo, kwa misingi ya umri, ulemavu, asili ya kitaifa, rangi, dini, jinsia, mwelekeo wa kijinsia, hali ya ndoa au uwezo wa kifedha kutengwa kushiriki, kunyimwa faida, au kufanyiwa ubaguzi katika mpango wowote wa elimu au shughuli yoyote inayosimamiwa au kuidhinishwa na Bodi ya Shule. Wafanyakazi wa Wilaya ya Shule ya Salem-Keizer watafanya jitihada endelevu za kutoa fursa sawa ya elimu kwa rufaa kwa mamlaka za utekelezaji wa sheria na watachukuliwa hatua za kinidhamu hadi ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule. Hii

hailengi kukatisha tamaa malezi ya, au uanachama katika, mashirika na shughuli ambazo si za jinai, za kupinga, za kibaguzi au zinazohusiana na wanafunzi wa shirika la genge na kuondoa hali hizo ambazo zinaweza kusababisha ubaguzi.

## KILA MWANAFUNZI ANAFANIKIWA (ESSA)

Mnamo Desemba 2015, Bunge la Amerika lilipitisha Sheria ya Kila Mwanafunzi Anafikiwa (ESSA), mfuko wa sheria ambao ulihuisha fursa na mahitaji kadhaa muhimu ya taarifa kwa wazazi na walezi wa wanafunzi walioandikishwa katika shule inayopokea fedha za shirikisho chini ya Title I, Sehemu A ya sheria hiyo. Ikiwa wewe ni mzazi au mlezi wa mwanafunzi aliyeandikishwa katika shule inayopokea fedha kutokaTitle I, una haki ya kuomba taarifa kuhusu sifa za kitaaluma ya mwalimu wa mwanafunzi wako na / au mtalaamu. Ikiwa unataka kufanya hivyo, tafadhali wasilisha ombi la maandishi la habari hii kwa mkuu wa shule ya mtoto wako. Maombi yaliyowasilishwa yatapokea majibu ya maandishi ndani ya siku kumi (10) za shule kuanzia tarehe ya kupokea. Taarifa zinazotolewa chini ya utaratibu huu zinalenga kuimarisha mawasiliano ya wazi na ya uwazi yaliyoanzishwa kati ya shule zetu na wanafunzi, wazazi, na jamii wanazozihudumia.

## PROGRAMU YA HUDUMA YA CHAKULA

Wilaya ya Shule za Salem - Keizer inashiriki katika programu za Kitaifa za Chakula cha Mchana na Kifungua Kinywa. Programu zote mbili zinasimamiwa na Idara ya Kilimo ya Marekani (U.S.D.A). USDA imeweka miongozo kwa wanafunzi wanaoshiriki labda chakula cha mchana au programu ya kifungua kinywa. Kwa chakula cha mchana, wanafunzi wanahimizwa kuchukua vipengele vyote vya chakula (nafaka, nyama/nyama mbadala, matunda, mboga, na maziwa) ya chakula kinachotolewa, lakini chini ya miongozo wa U.S.D.A, wanatakiwa tu kuchukua vipengele 3 kati ya 5 vya chakula, kimoja ikiwa angalau ½ kikombe cha matunda au mboga. Kwa kifungua kinywa, wanafunzi wanatakiwa kuchukua vitu 3 kati ya 4 vinavyotolewa vikiwa na vipengele 3 vya chakula (nafaka na chaguo la mbadala wa nyama / nyama inayoruhusiwa, matunda / mboga, na maziwa). Taarifa ya USDA/ODE: Taasisi hii ni mtoaji wa fursa sawa.

## UHURU WA KUJIELEZEA (INS-A029)

Shule za Umma za Salem-Keizer zinatambua kuwa kila mwanafunzi ana haki ya uhuru wa kujieleza na kuhimiza utekelezaji wa haki hii. Wanafunzi pia wana jukumu la kusaidia katika kudumisha shughuli za shule kwa utaratibu. Maafisa wa shule wana wajibu wa kuzuia usambazaji wa nyenzo au nyenzo zisizofaa ambazo zitavuruga wazi mchakato wa elimu. Machapisho ya wanafunzi yatakuwa huru dhidi ya ubaguzi, unyanyasaji, chuki na ubaguzi wa rangi. Kwa hiyo, machapisho na hotuba za wanafunzi zinafanyiwa mapitio na kuidhinishwa na uongozi wa shule. Uhakiki huo utafanyika bila kuchelewa. Mkuu wa shule ni mhariri na mchapishaji wa machapisho yote ya shule.

## VIKUNDI VYA UHALIFU

Vikundi vya uhalifu vinafafanuliwa kama kundi la watu watatu au zaidi ambao wanachama wao wana jina moja, alama, au rangi; na wanaojihusisha na vitendo vya uhalifu kama moja ya shughuli zao. Vikundi kama haya havitavumiliwa katika shule za wilaya. Mwanafunzi yeyote atakayepatikana akitumia namna au njia yoyote katika kuwakilisha genge, kuajiri wanachama wa genge lenye uwezo, kukuza uanachama wa genge au shughuli, kukiuka Sera za Kanuni ya Wilaya, au kujihusisha na shughuli zozote za genge la uhalifu, atapelekwa kwenye mamlaka za utekelezaji wa sheria na atachukuliwa hatua za kinidhamu na ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule. Hii hailengi kukatisha tamaa katika kuunda uanachama, makundi na shughuli ambazo sio za jinai, za kupinga, za kibaguzi au zinazohusiana na kundi la genge.

## UNYANYASAJI, VITISHO, UONEVU, UONEVU KWENYE MTANDAO NA KUTISHA (INS-A003)

Vitendo vya unyanyasaji, unyanyasaji wa kijinsia, vitisho, uonevu, unyanyasaji wa kimtandao na kutisha havitavumiliwa na mwanafunzi kwa mwanafunzi, wafanyakazi kwa mwanafunzi, au mwanafunzi kwa wafanyakazi. Unyanyasaji, vitisho, na uonevu vinaweza kutegemea, lakini sio tu, hadhi ya mtu kwa kundi linalolindwa limeelezewa katika Sera ya Utawala INS-A003. Wanafunzi wanahimizwa kuripoti wasiwasi kwa kukamilisha fomu ya ripoti ya siri kwa wanafunzi (INS-F030) iliyoko katika ofisi ya shule, maktaba, na kituo cha ushauri nasaha. Wazazi, walezi na wanajamii wanaweza kuwasilisha malalamiko yao kwa kukutana na uongozi wa shule au kwa utaratibu wa kutatua malalamiko rasmi kama inavyoainishwa katika sera ya Wilaya (ADM-A005) na utaratibu (ADM-P008). Mtu anaweza kutoa ripoti bila kujitambulisha moja kwa moja kwa mkuu wa shule. Ripoti zote zitachunguzwa na msimamizi wa shule. Mtu anaweza kuomba mapitio ya hatua zilizochukuliwa na wafanyakazi katika kujibu na / au kuchunguza ripoti kwa kuwasilisha ombi la maandishi kwa Mkuu wa mashule.

Wanafunzi ambao tabia zao zitabainika kukiuka sera hii watachukuliwa hatua za kinidhamu. Kulipiza kisasi au kulipiza kisasi dhidi ya mtu yeyote anayefanya kazi kwa nia njema katika mchakato wa malalamiko ni ukiukwaji wa sera ya wilaya. Mwanafunzi atakayebainika kumtuhumu mwingine kwa uongo kama njia ya kulipiza kisasi, au njia ya kuzimia, kunyanyaswa, vitisho, uonevu, unyanyasaji wa kimtandao au kutisha, atachukuliwa hatua za kinidhamu.

## WANAMICHEZO WA HIGH SKULI (INS-A014)

Wanamichezo wa high skuli wanatarajiwa kuzingatia Sera zote za Wilaya. Sera zinazohusisha matumizi ya tumbaku, pombe na madawa ya kulevya, kuanzia siku ya kwanza mwamichezo kuanza kushiriki katika michezo na kuendelea katika mwaka mzima wa shule na miaka yote inayofuata ya ushiriki wa rmichezo katika shule za Salem-Keizer. Sera hii inatekelezwa kwa masaa 24 kwa siku, hadi mwisho wa kila mwaka wa shule. Wanamichezo watakaokiuka sera hizi watakabiliwa na adhabu sawa na wanafunzi ambao hawashiriki katika michezo, na pia kusimamishwa mara moja kwa muda usiopungua wiki tatu kutoka kwenye mashindano ya michezo, na watafanyiwa tathmini ya madawa za kulevya baada ya kosa la kwanza. Wanamichezo wa high skuli wanatakiwa kudumisha wastani wa kiwango cha alama 2.0 kwa kila ripoti ya maendeleo ili kustahili kushiriki katika shuguli zote za michezo kama ilivyoandikwa katika Sera ya Wilaya ya Shule za Salem Keizer INS-A014, inayohusiana na Matarajio ya Wanafunzi Wachezaji: High Skuli.

## MAKABATI YA KUHIFADHIA & UKAGUZI WA MALI BINAFSI

Makabati ya kuhifadhia vitu na madawati ni mali ya wilaya ya shule na yanadhibitiwa na uongozi wa shule, wanafunzi wanaruhusiwa kuyatumia. Kama shule zina wasiwasi kuhusu matumizi ya makabati ya kuhifadhia vitu kwa kuhifadhi vitu visivyo halali na pia zina wasiwasi kuwa makabati ya kuhifadhania vitu yanatunzwa siipasavyo. Kulingana na kiwango cha tuhuma, mali ya kibinafsi inaweza kukaguliwa na makabati ya kuhifadhia yanaweza kufunguliwa kwa hiari ya msimamizi wa jengo kwa njia ya busara, wakati unaofaa, na kwa njia inayofaa.

## MAGARI

Wanafunzi wa shule ya high skuli wanaweza kuendesha magari kwenda na kutoka shuleni. Na Baadhi ya kanuni za shule, hata hivyo, sababu ya upungufu wa nafasi za maegesho ya magari, kwa kujali usalama, ulinzi wa mali, na usumbufu wa programu ya shule. Ada ya maegesho inaweza kutathminiwa na wilaya. Hakuna magari ya wanafunzi yatakayoruhusiwa kuondoka katika viwanja vya shule wakati wa muda wa masomo, ikiwa ni pamoja na saa ya chakula cha mchana, bila ruhusa ya mkuu wa jengo. Ruhusa ya kuendesha gari inaweza kufutwa wakati wowote kama ukikiuka kanuni yoyote ya shule kuhusu matumizi ya gari. Hakuna mwanafunzi wa sekondari atakaye ruhusiwa kuendesha gari kwenda shuleni.

Wazazi wana jukumu la kusajili gari na ofisi ya shule kabla ya mwanafunzi wao kuendesha gari shuleni. Wanafunzi ambao wana umri wa miaka 18 au kujitegemea/kuachiliwa lazima wasajili magari yao na shule. Wanafunzi hao watafuata sheria na kanuni zinazosimamia matumizi ya magari hayo katika kipindi ambacho mwanafunzi yuko chini ya uongozi wa shule.

## KAULI ISIYO YA UBAGUZI

Ni sera na kipaumbele cha Wilaya ya Shule ya Salem-Keizer kwamba hakutakuwa na ubaguzi au unyanyasaji wa watu au vikundi kwa misingi ya rangi, dini, jinsia, mwelekeo wa kijinsia, utambulisho wa kijinsia, usemi wa kijinsia, asili ya kitaifa, hali ya ndoa, umri, hali ya ukongwe , habari za maumbile au ulemavu katika programu zetu za elimu, shughuli au ajira.

Title IX ni sheria ya haki za kiraia ambayo ilipitishwa mwaka 1972 ili kuhakikisha kuwa wanafunzi na wafanyakazi wanatendewa sawa na kwa haki katika mazingira ya elimu bila kujali jinsia zao. Sambamba na Title IX, Wilaya ya Shule za Salem-Keizer inakataza ubaguzi kwa misingi ya jinsia, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kijinsia, katika programu na shughuli zote za elimu.

Wilaya ya Shule ya Salem-Keizer imedhatiti kuhakikisha kuwa malalamiko yote ya ubaguzi, unyanyasaji wa kijinsia na ukatili wa kijinsia yanachunguzwa kwa kina.

Malalamiko na maswali kuhusu ubaguzi, ikiwa ni pamoja na ubaguzi wa kijinsia na Title IX, yanaweza kuwasilishwa moja kwa moja kwa **uongozi wa shule au** Wilaya ya Shule za Salem-Keizer**:** **Mratibu wa Title IX** John Beight, Mkurugenzi Mtendaji wa Rasilimali Watu / Mratibu wa Title IX: 2450 Lancaster Drive NE, Salem, OR 97305; 503.399.3061; beight_john@salkeiz.k12.or.us.; www.salkeiz. k12.or.us.

## MAJUKUMU YA MWANAFUNZI KWENDA NA KUTOKA SHULE (INS-A001)

Shule inajali usalama na mwenendo wa wanafunzi wanapokwenda na kutoka shuleni na kwa ajili ya ulinzi wa mali za jirani. Wanafunzi wote wanaokwenda na kutoka shuleni wanatakiwa kuwa na udhibiti mzuri wa shule na Sera ya Nidhamu ya Wilaya na Utawala.

## HAKI YA KUPITIA TAARIFA ZA MWANAFUNZI

Mzazi au watu wengine katika uhusiano wa wazazi na pia wanafunzi wanaostahili kama ilivyoandikwa katika Utaratibu wa Wilaya INS-P022, wana haki ya:

1. Kukagua na kupitia rekodi za mwanafunzi.
2. Kuomba marekebisho ya rekodi za elimu ili kuhakikisha kuwa si sahihi, zinapotosha, au zinakiuka usiri wa mwanafunzi na haki zake.
3. Ridhaa ya kutoa taarifa binafsi zinazotambulika zilizomo kwenye rekodi za elimu ya wanafunzi, isipokuwa kwa kiwango ambacho sera hii inaruhusu kutolewa kwa taarifa bila idhini.
4. Kwa mujibu wa utoaji wa Kanuni ya Utawala ya Oregon 581-021-0410, jalada na Idara ya Elimu ya Amerika in malalamiko yanayodai kuwa wilaya hiyo imeshindwa kuzingatia Sheria ya Haki za Elimu ya Familia na Faragha.
5. Kupata nakala ya Utaratibu wa Wilaya INS-P022. Sera kamili inaweza kuonekana katika kila shule, Ofisi ya Mkuu wa mashule na kwenye tovuti ya wilaya.

Mzazi au mtu mwingine katika uhusiano wa wazazi au mwanafunzi anayestahili ambaye anataka kukagua rekodi za elimu atawasilisha ombi lake kwa mkuu wa jengo au mtu aliyeteuliwa.

## MAHUDHURIO YA SHULE (INS-A009)

Shule za Umma za Salem-Keizer zimejidhatiti kutoa elimu bora kwa wanafunzi wote. Uwiano mkubwa upo kati ya mafanikio ya kitaaluma ya mwanafunzi shuleni na mahudhurio yao ya kila siku. Mwanafunzi anatarajiwa kuwepo darasani kipindi chochote cha masomo ili kufikia malengo ya darasa.

Kwa upande wa mahudhurio, mwanafunzi anakuwepo au hayupo. Kukosekana kwa kisingizio ni kile ambacho kinaidhinishwa na mkuu shule au mtu aliyeteuliwa ni moja katika hizi zifuatazo:

- Ugonjwa wa mwanafunzi;
- Ugonjwa mbaya katika familia;
- Maelekezo ya kidini (yenye kizuizi kwa ORS.339.420;
- Mwelekeo wa hali ya hewa;
- Miadi ya matibabu au uteuzi wa mahakama;
- Hali ya dharura, udhuru ulitolewa, au kutokana na mazingira;
- Wanafunzi ambao wazazi/walezi wao ni wanachama wa jeshi na wako Jeshi la Amerika.

Kukosekana shule ni kile ambacho hakina kisingizio wala sio rasmi, na kinaweza kusababisha hatua za kinidhamu.

Kukosekana lazima kuwe na kisingizio cha mzazi au mlezi wa mwanafunzi. Ili kudumisha usalama wa wanafunzi, wilaya inatakiwa kuwasiliana moja kwa moja na wazazi au walezi wakati ambapo mwanafunzi hatakuwepo.

Kila mkuu wa shule au mtu aliyeteuliwa atatengeneza na kutekeleza sera na utaratibu wa mahudhurio unaojumuisha matarajio ya mahudhurio ya wanafunzi kwa kuhimiza mahudhurio hayo. Kila shule itatengeneza na kutekeleza sera ya kuchelewa. Mzazi au mlezi atajulishwa na wilaya kama mwanafunzi amekosa shule na kutokuwepo kwake hakujafutwa. Rufaa ya hatua za

kinidhamu zilizochukuliwa kutokana na kutokuwepo bila kutarajiwa zinaweza kutolewa kupitia mchakato wa malalamiko ya wilaya.

Kwa kuongezea, msimamizi wa shule au aliyeteuliwa atamjulisha mzazi au mlezi juu ya mahudhurio yasiyo ya kawaida ya mwanafunzi au mahudhurio yasiyo mara kwa mara. Ikiwa hajahudhuria (kushindwa kuhudhuria shule) au mahudhurio yasiyo ya kawaida (kutokuwepo kwa siku nane bila na nusu siku au kulingana na, katika kipindi cha wiki nne) tatizo linaendelea, msimamizi wa shule au aliyeteuliwa, atatoa taarifa ya maandishi kwa mtu au kwa barua iliyosajiliwa au kuthibitishwa kwa mzazi au mlezi kwamba mwanafunzi lazima aonekane shuleni siku inayofuata baada ya kupokea taarifa na aendelee kuhudhuria kila siku kwa kipindi cha mwaka kilichobakia.

Iwapo taarifa hiyo hapo juu haitafuatwa, mkuu shule au aliyeteuliwa, chini ya masharti ya ORS 339.925, atatoa taarifa kwa maandishi (iliyoandikwa kwa lugha ya asili ya mzazi) kwa mzazi au mlezi kwamba: Mzazi au mlezi na mtoto lazima ahudhurie mkutano na msimamizi wa shule aliyeteuliwa kujadili hali hiyo; mzazi au mlezi anapaswa kumwandikisha mtoto wake na kuhakikisha kuwa mwanafunzi anasoma shule muda wote na kila siku ; Kushindwa kujiandikisha, kutuma, na kuhakikisha mtoto ana mahudhurio ya mara kwa mara ni ukiukwaji wa Class C.

Ikiwa shida ya mahudhurio yasiyo ya kawaida au isiyo ya kawaida inaendelea, Mkuu wa mashule au mtu aliyeteuliwa anaweza kuchagua kutoa adhabu kwa mujibu wa ORS 339.925. Ikiwa ni utoro ulioshindakana na nje ya udhibiti wa mzazi au mtu katika uhusiano wa wazazi, suala hilo litapelekwa kwa mamlaka ya vyombo vya sheria kwa vijana.

## UPEKUZI NA KUKAMATA (INS-A015)

Maafisa wa shule wana mamlaka ya kufanya upekuzi wa mali za wilaya na mali binafsi za wanafunzi kulingana na tuhuma, na kukamata vifaa visivyoruhusiwa, visivyo halali au visivyo salama, na / au kutambua hali isiyo salama kama hatua madhubuti ya kuweka shule salama. Wakati wowote iwezekanavyo, upekuzi utafanyika kwa idhini ya mwanafunzi na mbele yao.

Ikiwa vifaa visivyoidhinishwa, visivyo halali au visivyo salama vitagunduliwa wakati wa aina yoyote ya upekuzi, maafisa wa shule watatumia moja au chaguzi zote zifuatazo: Kukamatwa kwa magendo; kutoa taarifa kwa mamlaka husika; kufuata sera na utaratibu wa nidhamu wa wilaya. Ambapo wanafunzi wanahudhuria shughuli za wanafunzi ambazo zinachukuliwa kama ni upendeleo kama vile dansi za shule, iwe ndani au nje ya shule; shule inaweza kuwapima wanafunzi na wageni kama wamekunywa pombe kabla ya kuruhusiwa kuingia ndani.

Kila mwaka, wazazi, wanafunzi, wafanyakazi na jamii watajulishwa kuwa wilaya inaweza kufanya upekuzi na mbwa kwenye mali ya shule na ikiwa maafisa wa shule wana tuhuma za kuweza kuamini kuwa kuna magendo shuleni, upekuzi na mbwa unaweza kufanywa bila kupangwa.

## KUPATA ELIMU MAALUM YA MTOTO

Wanafunzi wote, wanaozaliwa hadi umri wa miaka 21 wanaweza kustahili huduma maalum za elimu. Wanafunzi wanastahili chini ya miongozo iliyowekwa na sheria ya serikali na kuelekezwa na kila jimbo na Idara ya Elimu. Wilaya za shule zinapaswa kutambua, kutafuta na kutathmini watoto wote wakazi wenye ulemavu, bila kujali ukali wa ulemavu, ambao wanahitaji kuangaliwa mapema, elimu maalumu ya utotoni au huduma maalum za elimu.

Pale mwanafunzi anapopewa rufaa ya elimu maalum, tathmini inaweza kupendekezwa. Rufaa zote huanzia katika shule ya jirani. Wafanyakazi waliofunzwa watakamilisha uchunguzi, kufanya tathmini ya uchunguzi na kukusanya taarifa kutoka vyanzo mbalimbali. Tathmini zote za awali hufanywa kwa idhini iliyosainiwa na mzazi na / au mlezi. Taarifa kutoka kwa ya mzazi / mlezi huzingatiwa katika hatua zote za kutathmini, ustahiki na uwekaji.

## MWANAFUNZI KUHOJIWA NA POLISI (INS-A033)

Maafisa wa vyombo vya usalama wanaweza kumhoji mwanafunzi katika eneo la shule. Mamlaka ya shule inaweza kujaribu kuwajulisha wazazi au walezi juu ya kitendo hicho kwa idhini ya maafisa wa uchunguzi tu.

## MADAI NA ADA KWA MWANAFUNZI (INS-A012)

Wanafunzi na wazazi / walezi wao watawajibika kifedha kwa vifaa vyovyote vilivyopotea au kuharibiwa kwa makusudi. Wilaya itafuatilia ukusanyaji wa madeni kwa kiwango kamili kinachoruhusiwa na sheria ya Jimbo la Oregon. Kutolipa ada, faini, na / au kurejeshwa kwa mali iliyoharibiwa / iliyopotea inaweza kusababisha: Kupoteza fursa ya ushiriki wa mwanafunzi na / au kuhudhuria shughuli za shule na / au shughuli zisizo za kitaaluma ikiwa ni pamoja na lakini sio tu sherehe na / au shughuli zinazohusiana na mahafali ya kuhitimu, matukio ya michezo, na shughuli zinazodhaminiwa na shule kama sherehe na burudani (ikijumuisha dansi)

Wilaya inaweza kuchukua hatua za kisheria, ikiwa ni pamoja na rufaa ya kiasi cha makusanyo ambayo hayakusanywa au kwa kuwasilisha malalamiko ya wananchi katika Mahakama ya Mkazi baada ya kutoa notisi kama inavyotakiwa katika ORS 339.270.

## UTORO NA AMRI YA KUTOTOKA NJE WAKATI WA MCHANA

Salem ina amri ya kutotoka nje mchana na Keizer ina sheria ya utoro ambayo inazuia mtoto (kati ya umri wa miaka 5 na 18) kuwa katika maeneo ya umma wakati wa saa za kawaida za shule ili kupunguza utoro na/au kiwango cha uhalifu. Mahudhurio yasiyo ya kawaida yakatokea, wilaya itachunguza, kutuma taarifa ya mahudhurio yasiyo ya kawaida kwa mzazi au mtu mwingine katika uhusiano wa wazazi, na kuamua ni hatua gani za kurekebisha zinapaswa kuchukuliwa. Wilaya inaweza kuendelea na hatua za kisheria kwa mujibu wa sheria za jimbo, ikiwa ni pamoja na rufaa kwa vyombo vya sheria kwa kutoa faini kufikia kiwango cha hadi dola 500.

*Miongozo inaendelewa kupitiwa na kurekebishwa.*
*Mtumiaji wa miongozo anatakiwa kupitia tovuti ya QAM kwa toleo la hivi karibuni.*